
Toleo Na. 1 | 2020-2021

# JARIDA LA WAKILI MKUU



## WAKILI MKUU WA SERIKALI:

# TUMEOKOA MATRILIONI





ZIARA YA ALIYEKUWA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA KATIKA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

# BODI YA WAHARIRI




**DR. BONIPHACE NALIJA LUHENDE**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali
**MWENYEKITI**



**INNOCENT P.M. MUNGY**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano
**MHARIRI**



**DENNIS JULIUS BUYEKWA**
Afisa Habari
**MHARIRI WA HABARI**



**NYAMHONI ROBERT CHACHA**
Afisa TEHAMA
**MSANIFU WA MAUDHUI**

**WAJUMBE**



**GEORGE NATHANIEL MANDEPO**
Mkurugenzi wa Usuluhishi



**KIUYE MBWANA SHEMAKAME**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti



**ABUBAKAR AMIN MRISHA**
Mkurugenzi Msaidizi - Usimamizi wa Mashauri

# YALIYOMO


4. WAZIRI NCHEMBA AIPONGEZA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KWA KUZIISHI NDOTO ZA MHE. RAIS MAGUFULI

6. SERIKALI YAOKOA SHILINGI BILIONI 10 ZA KITANZANIA KWA KUTUMIA MAWAKILI WAKE

10. ACACIA YAKIRI KUWA KESI WALIYOFUNGUA DHIDI YA SERIKALI NI MWIBA KWAO: WAIONA BARRICK NI MKOMBOZI KWA KUINUNUA

12. SERIKALI YASHINDA KESI YA RUFAA YA KUFUTWA KWA KIFUNGU CHA 148 (5) CHA SHERIA YA MWENENDO WA MASHAURI YA JINAI

13. SERIKALI YAMGALAGAZA TUNDU LISSU MAHAKAMANI

14. MAWAKILI WA SERIKALI WATAKIWA KUSIMAMIA MASHAURI KWA KUFUATA SHERIA, KANUNI NA MIONGOZO

16. PROF. MCHOME AHIMIZA UWAZI NA USHIRIKISHWAJI KATIKA UTENDAJI OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

18. MAMA SAMIA: NITABORESHA MASLAHI YA WATUMISHI

20. PROF. KILANGI ATAKA MAWAKILI NCHINI KUJINOA KILA UCHAO

22. WAZIRI KABUDI: TOENI TAARIFA KWA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

24. WAKILI MKUU WA SERIKALI AKUMBUSHWA KUZINGATIA KANUNI, TARATIBU, MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA




OSG OFFICE BUILDING

# WAZIRI NCHEMBA AIPONGEZA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KWA KUZIISHI NDOTO ZA MHE. RAIS MAGUFULI

Na Innocent P.M. Mungy




Aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba ameipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya katika kusimamia kikamilifu mashauri mbalimbali yanayofunguliwa dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

Waziri Nchemba ametoa pongezi hizo mapema leo, tarehe 04 Agosti 2020 wakati akizungumza na wajumbe wa Menejimenti wa ofisi hiyo katika kikao kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano uliopo ndani ya viwanja vya ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.

Amesema kuwa matokeo ya kuanzishwa kwa Ofisi hiyo yameleta tija kwa Taifa kwani uwepo wa Ofisi hiyo umesaidia kuokoa takribani shilingi Trioni 11.4 kiasi cha fedha ambacho kingelipwa iwapo serikali ingeshindwa katika mashauri hayo.

“Rais wetu Mhe. Magufuli aliona mbali ndio maana aliamua kuanzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, kwa muda mfupi mmethibitisha umuhimu wa Ofisi hii kwa kuokoa shilingi Trioni 11.4”, amesema Mhe. Waziri.

Katika kuhakikisha maslahi ya watanzania yanalindwa ipaswavyo Mhe. Waziri amewataka watumishi wa Ofisi hiyo hususani mawakili kuhakikisha wanafanya kazi kubwa ili kuhakikisha tunashinda kila vita ya uchumi itakayopiganwa dhidi yetu.

“Vita vya kiuchumi havipiganwi hadharani, vita vya kiuchumi vinapiganwa kisheria hivyo linapokuja suala la maslahi ya nchi tunaupande mmoja tu nao ni kuipigania nchi yetu”, alisema Mhe. Nchemba.

Ameongeza kuwa kwa kutimiza majukumu yetu ipasavyo kutaisaidia nchi yetu kuendelea kupiga hatua za kimaendeleo kwa vile malengo aliyonayo Rais wetu Mhe. John Pombe Magufuli ni kuhakikisha tunalinda rasilimali za nchi yetu kwa nguvu zote. Hivyo hakikisheni tunamsaidia kuokoa mali za watanzania, amesema



kuwa watanzania tunayo bahati ya kuwa na Rais

mzalendo kuhu akibainisha ukweli kuwa moyo wa Rais wetu unawaza maisha ya watanzania wakati wote ndio maana kila fedha inayookolewa na serikali imekuwa ikielekezwa kwenye shughuli za maendeleo hatua iliyopelekea nchi yetu kuingia katika uchumi wa kati kabla ya mwaka 2025.

Amesisitiza kuwa fedha ambazo zingelipwa huko, ndio fedha ambazo zinajenga na kuboresha miundombinu ikiwemo barabara, vituo vya afya, shule na miradi mikubwa ya reli ya kisasa pamoja na bwawa kubwa la kufua umeme katika mto Rufiji.

Akizungumza wakati wa kumkaribisha Waziri huyo, Naibu Katibu Mkuu wa wizara ya Katiba na Sheria Bw.Amoni Mpanju, ameipongeza Ofisi ya Wakili



Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwani hatua hiyo imesaidia kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kitasaidia nchi kuwekeza katika miradi mikubwa ya maendeleo.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali Bw. Gabriel Malata amemshukuru Mhe. Waziri kwa ziara hiyo ofisini hapo huku akiahidi kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika kuhakikisha ofisi hii inaendelea kusimamia na kuratibu mashauri yote ipasavyo.

Akielezea mafanikio yaliyopatikana Bw. Malata amesema kuwa kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kushinda mashauri mbalimbali ikiwepo mashauri yaliyofunguliwa katika nchi za Afrika Kusini na Kanada ambapo ilipelekea kuachiliwa kwa ndege za Shirika la Ndege la Tanzania zilizokuwa zimeshikiliwa katika nchi hizo.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli kwa tangazo la Serikali Na. 50 tarehe 12 Februari, 2018 ikiwa na jukumu la kusimamia, kuendesha na kuratibu mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayofunguliwa dhidi ya Serikali ya Tanzania ndani na nje ya nchi.



**“ Fedha ambazo zingelipwa huko, ndio fedha ambazo zinajenga na kuboresha miundombinu**





Na Dennis J. Buyekwa

# SERIKALI YAOKOA SHILINGI BILIONI 10 ZA KITANZANIA KWA KUTUMIA MAWAKILI WAKE

Katika kuhakikisha inaokoa fedha za uendeshaji wa mashauri, Serikali ya Tanzania imeahidi kuendelea kuwatumia Mawakili wake katika kuendesha na kusimamia mashauri mbalimbali yanayoikabili nje na ndani ya nchi.

Hayo yalizungumzwa na aliyekuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Ally Possi alipokuwa akizungumzia hatua zilizochukuliwa na Serikali katika shauri lililofunguliwa nchini Uholanzi na Kampuni ya Sunlodges BVI na Sunlodges Tanzania (L.T.D).

Katika Shauri hilo mlalamikaji ambaye ni kampuni ya Sunlodges BVI alikuwa akilalamikia hatua ya Serikali kufuta hatimiliki ya ardhi iliyokuwa inamilikiwa na mwekezaji huyo baada ya kushindwa kuiendeleza kwa shughuli za kilimo ambazo zilikuwa zimeainishwa kwenye hatimiliki ya shamba hilo.

Kufuatia hatua hiyo Serikali iliamua kuwatumia Mawakili hatua iliyosaidia Serikali kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ukilinganisha na kiasi kilichokuwa kinatumiwa na Serikali awali wakati walipokuwa wanatumia Mawakili binafsi.

Akizungumzia kiasi cha fedha kilichookolewa katika shauri hilo, Dkt. Possi alisema, Serikali kupitia Mawakili wake wamefanikiwa kutumia fedha kidogo ukiilinganisha na kiasi kikubwa cha fedha kilichokuwa kikitumika miaka ya nyuma pale Serikali iilipokuwa ikiajiri Mawakili mbalimbali hususani wale wa nje ya nchi.



Mkurugenzi wa Usuluhishi
**Ndg. George N. Mandepo**

Akiendelea kuzungumzia shauri hilo Dkt. Possi alisema hii ni mara ya kwanza kwa Serikali kutumia mawakili wake badala ya mawakili binafsi kutoka ndani na nje ya nchi

Dkt. Possi alisema kwa kutumia Mawakili wa ndani Serikali

imefanikiwa kuokoa fedha za kutosha kwani katika shauri hili pekee Serikali imetumia kiasi cha fedha za kitanzania shilingi milioni 700 tofauti na hapo awali ambapo serikali ilitumia mpaka Shilingi bilioni 10 za kitanzania.
"Zipo faida nyingi za kuwatumia mawakili wazawa, mathalani katika kesi hii tumeweza kuokoa fedha nyingi ambazo sasa zitaenda kuelekezwa kwenye mambo mengine ya kimaendeleo kwa manufaa ya wananchi" Alisema Dkt. Possi.
Katika hatua nyingine Dkt. Possi aliahidi kuendelea kuwapatia mafunzo



mawakili hao yatakayosaidia kuwajengea uwezo katika mashauri ya kimataifa, kitendo kitakacho wasaidia kuendelea kuiwakilisha vyema Serikali katika Mashauri mbalimbali yanayoikabili ndani na nje ya nchi.
Naye Mkurugenzi wa Idara ya Usuluhishi Bw. George Mandepo kwa niaba ya Mawakili wa Serikali aliipongeza Serikali kwa uamuzi huo wa kutumia Mawakili wa Serikali sio tu itasaidia kuokoa kiasi kikubwa cha fedha bali pia itasaidia Serikali katika masuala nyeti ikiwa ni pamoja na kutunza siri za Serikali hasa katika yale mashauri yenye maslahi mapana kwa Taifa, lakini pia itasaidia kuwapa uzoefu mawakili wa Serikali katika mashauri mbalimbali hususani yake ya kimataifa.
Serikali ya Tanzania imeamua kuanza kutumia Mawakili wake katika kuendesha mashauri mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli katika kubana matumizi hatua itakayosaidia kuchochea kasi ya maendeleo katika sekta nyingine kwa manufaa ya taifa kwa ujumla.

**"Katika picha, Mawakili wa Serikali.**




*Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akiongea na wananchi alipohudhuria katika kilele cha Maadhimisho ya wiki ya Sheria na miaka 100 ya Mahakama ya Tanzania wa kwanza kulia ni Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi Pamoja na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba. Kilele cha Maadhisho hayo kilifanyika katika Viwanja vya Chinangali Vilivyopo Jijini Dodoma.*



*Aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Mkuungano wa Tanzania ambae sasa ni Rais wa Jamhuri ya Mkuungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan katikati, akizindua miongozo na kanuni mbalimbali za uendeshaji wa Shughuli za Mahakama kuashiria kufunguliwa kwa mwaka mpya wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Uzinduzi huo ulifanyika wakati wa Maadhimisho ya wiki ya Sheria na miaka 100 ya Mahakama ya Tanzania katika viwanja vya Nyerere square vilivyopo katikati ya jiji la Dodoma.*




***Watumishi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa wameshika Bango la ofisi hiyo tayari kwa kuanza matembezi ya kilomita tano, kuelekea ufunguzi wa Wiki ya Sheria na Miaka 100 ya Mahakama ya Tanzania yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali vilivyopo Jijini Dodoma***




***Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geofrey Mizengo Pinda akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kutembelea banda la Wakili Mkuu wa Serikali katika Maadhimisho ya Wiki ya Sheria na Miaka 100 ya Mahakama ya Tanzania. Maadhimisho hayo yalifanyika katika viwanja vya Nyerere square vilivyopo katikati ya Jijina la Dodoma.***

# MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA



# ACACIA YAKIRI KUWA KESI WALIYOFUNGUA DHIDI YA SERIKALI NI MWIBA KWAO: WAIONA BARRICK NI MKOMBOZI KWA KUINUNUA

Na Dennis J. Buyekwa

Kitendo cha Kampuni ya Acacia, kusitisha usikilizwaji wa mgogoro wa muda mrefu kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni mbili za Madini za Pangea Minerals Limited na Bulyanhulu Gold Mining Ltd za hapa Tanzania kinahesabika kuwa ni hatua ya Kampuni hiyo kusalimu amri katika mgogoro huo mkubwa.

Mnamo tarehe 19 Julai 2019, Kampuni ya Acacia Mining plc – ambayo imeorodheshwa kwenye soko la hisa la London, Uingereza, iliomba kusitishwa kwa shauri lililopangwa kusikilizwa kuanzia tarehe 22 Julai, 2019 katika Mahakama ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kimataifa ya London (LCIA) ambapo upande wa Tanzania ulikuwa umejiandaa vyema kupitia Mawakili wake wa Serikali kutetea kesi hiyo.

Kampuni ya Acacia, pamoja na kutosajiliwa Tanzania, kwa muda mrefu imekuwa ikidai kuzimiliki kampuni mbili za uchimbaji madini za Pangea Minerals Limited na Bulyanhulu Gold Mining Limited. Acacia ilizishawishi kampuni hizo zifungue mgogoro wa usuluhishi dhidi ya Serikali ya Tanzania katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro nchini Uingereza.

Mnamo mwezi Machi 2017, Serikali ya Tanzania iliamua kupiga marufuku usafirishaji wa makinikia ya madini kwenda nje ya nchi. Marufuku hiyo ililenga kuchochea uongezaji thamani na uwazi katika mnyororo wa thamani katika sekta ya madini nchini Tanzania. Katika hatua hii, makontena 277 ya madini ya kampuni za Pangea Minerals Limited na Bulyanhulu Gold Mining Limited yalishikiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokana udanganyifu wa Kampuni hizo.

Kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali kuzuia makontena Bandarini, kampuni hizo za Pangea Minerals Limited na Bulyanhulu Gold Mining Limited zilifungua mashauri kupinga uamuzi wa TRA wa kuzuia usafirishaji wa makinikia nje ya nchi.

Aidha, Julai, 2017, Acacia walifungua mgogoro wa Kimataifa katika Mahakama ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kodi (TRAB) na LCIA wakilalamikia Serikali ya Tanzania kuwa imevunjwa Mikataba ya Uchimbaji Madini (MDAs).

Hata hivyo, mambo hayakuindea vizuri Acacia ambapo mnamo tarehe 22 Februari 2019 shauri lililofunguliwa na Kampuni yake ya Bulyanhulu Gold Mining Limited lilitupiliwa mbali na Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB) hapa nchini. Bodi ya Rufaa ilikubaliana na hoja za upande wa Serikali kuwa marufuku ya kusafirisha makinikia nje ya nchi haya kuwa sahihi kwa mujibu wa Sheria za Kodi za Tanzania.

Baada ya maamuzi ya TRAB, ambayo hayakuiridhisha Acacia, kampuni hiyo ilibakiwa na njia moja tu ya kutatua mgogoro huo, ambayo ni kupitia Mahakama ya Kimataifa nchini Uingereza.

Kwa upande wa Serikali, kesi iliyofunguliwa kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Migogoro ilisimamiwa na kuendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, kabla ya kesi hiyo kuanza kusikilizwa siku ya tarehe 22 Julai 2019, Mawakili wa Makapuni ya Acacia waliitaarifu Serikali ya Tanzania kusudio la kusitisha usikilizwaji wa kesi hiyo ili kuruhusu kampuni ya Barrick Gold Corporation kukamilisha majadiliano yanayoendelea kati yake na Serikali ya Tanzania.

Hata hivyo, kupitia taarifa iliyotolewa na Mtendaji Mkuu wa Acacia Bw. Peter Geleta mnamo tarehe 19 Julai 2019, imethibitika pasipo shaka kuwa kampuni hiyo ilikuwa imeomba kusitishwa kusikilizwa kwa shauri hili ili kuipa nafasi kampuni ya Barrick kukamilisha ununuzi wa hisa zote za Acacia zilizokuwa zinamilikiwa na wanahisa wadogo. Maelezo hayo yanathibitisha wazi kuwa, Acacia hawakuwa na uwezo

wa kushinda kesi hiyo na ndio maana wakakubaliana kirahisi na kampuni ya Barrick kununuliwa baada ya mvutano wa muda mrefu. Ujumbe ulioandikwa na Peter Geleta ambao umelengwa kwa wafanyakazi wa Acacia, umewasihi wafanyakazi kuwa watulivu ili kusubiri kukamilika kwa majadiliano kati ya Kampuni ya Barrick na Tanzania ambapo Mtendaji Mkuu huyo wa Acacia ameeleza wazi kuwa itatoa nafuu kwa hali ya sasa ya Kampuni na wafanyakazi na kumaliza kabisa mgogoro wa kikodi uliokuwepo.

Itakumbukwa kuwa, Acacia waliwahi kutoa tamko kuwa hawatambui majadiliano yanayoendelea kati ya Kampuni ya Barrick na Tanzania. Kitendo cha sasa cha Acacia kukubali kununuliwa na kuruhusu Barrick kuendelea na mazungumzo na Tanzania kinathibitisha dhahiri kuwa, madai ya Acacia dhidi ya Serikali ya Tanzania hayakuwa na msingi wowote.

Kwa Acacia kuridhia kuwa kesi iliyopo Mahakamani isitishwe ni moja ya uthibitisho kuwa utaratibu uliotumika na Tanzania kushughulikia ubadhirifu katika Sekta ya Madini nchini ulikuwa na manufaa kwa Taifa.

Kukamilika kwa mauziano ya hisa kunatoa nafasi kwa Serikali ya Tanzania kufikia muafaka na kampuni ya Barrick, na hivyo kuleta mwanzo mpya katika sekta ya madini nchini Tanzania ambapo kimsingi utaiwezesha Tanzania ambayo awali haikuwa mwanahisa katika Mikataba ya Madini (MDA) kuwa mmoja wa wanahisa kwenye Kampuni ya pamoja itakayoanzishwa kwa ubia.

Aidha, hatua hiyo itawezesha Serikali kuweza kusimamia kwa uthabiti faida inayotokana na madini hapa nchini tofauti ilivyokuwa awali.

> “ ACACIA WAIONA BARRICK NI MKOMBOZI KWA KUINUNUA



**Mawakili wa Serikali wakiwa kwenye majadiliano muda mchache kabla ya kuanza kusikilizwa kwa shauri**

# SERIKALI YASHINDA KESI YA RUFAA YA KUFUTWA KWA KIFUNGU CHA 148 (5) CHA SHERIA YA MWENENDO WA MASHAURI YA JINAI

Na Innocent P.M. Mungy




Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es salaam, Wakili Mkuu wa Serikali Bwana Gabriel Pascal Malata.

Serikali imeshinda kesi ya rufaa ya kufutwa kwa kifungu cha 148 (5) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania inayozuia dhamana kwa makosa makubwa. Kifungu hicho kinazuia dhamana kwa makosa ya jinai yakiwemo ya utakatishaji fedha haramu, mauaji, uhaini, unyang'anyi wa kutumia silaha na usafirishaji haramu wa binadamu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es salaam, Wakili Mkuu wa Serikali Bwana Gabriel Malata, amesema kuwa Mahakama ya Rufaa mnamo tarehe 5 Agosti 2020, imekubaliana na rufaa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo ilikuwa ikipinga maamuzi ya Mahakama Kuu yaliyotolewa na jopo la majaji watatu kwa kutamka ya kuwa kifungu cha 148 (5) cha Mwenendo wa Mashauri ya Jinai kinakinzana na matakwa ya Sura ya 13 (6) (b) na 15 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa.

Hukumu hiyo ilitolewa na Mahakama Kuu katika kesi namba 29 ya 2019 iliyofunguliwa na wakili wa kujitegemea Bwana Dickson Paulo Sanga dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika kesi hiyo Bwana Sanga alitaka Mahakama Kuu kufuta kifungu cha 148 (5) kwa kuwa kinakinzana na Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania ambapo mahakama Kuu iliridhia maombi yake.

"Katika rufaa iliyokatwa na Serikali ilipinga maamuzi ya Mahakama Kuu. Mahakama ya Rufaa ambayo iliketi tarehe 6 Julai 2020, pamoja na mambo mengine ilisikiliza hoja za Serikali, kwamba Kifungu cha 148 (5) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania haikinzani na Ibara ya 13 (6) na 15 (1) (2) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" alisema Bwana Malata.

"Serikali ilieleza kuwa kifungu hicho cha Sheria kinalenga kutekeleza Ibara ya 13 (3) inayofafanua juu ya misingi ya haki, uhuru na wajibu wa mtu na kwamba haki, uhuru na wajibu unatekelezwa kwa kuzingatia Sheria zingine za nchi na haki, uhuru na haki ya watu wengine".

Amesema kwa kuzingatia hayo, Mahakama ya Rufaa imefuta hukumu ya Mahakama Kuu na kueleza kuwa Kifungu cha 148 (5) (a) (i), (ii), (iii), (b), (c), (d) na (e) Sheria ya Mwenendo wa Jinai Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania hakikinzani na Ibara ya 13 (3) na 15(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania badala yake kinalenga katika kuwezesha utekelezaji mzuri wa Ibara ya 30 (2) inayolenga katika kuhakiksha kwamba haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma haviathiriwi na matumizi mabaya ya uhuru na haki za watu binafsi na pia kuhakikisha ulinzi, usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii, afya ya jamii na utekelezaji mzuri wa mipango ya maendeleo ya jamii.

# SERIKALI YAMGALAGAZA TUNDU LISSU MAHAKAMANI

Na Innocent P.M. Mungy



Mahakama kuu ya Tanzania kanda ya Dar es Salaam imetupilia mbali maombi ya aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Singida Mashariki kwa tiketi ya Chama cha Maendelo na Demokrasia (CHADEMA) Mhe. Tundu Lissu.

Katika maombi hayo namba 42 ya mwaka 2019, mlalamikaji alikuwa akiomba ridhaa Mahakama Kuu ili imruhusu kukata rufaa kwa lengo la kupinga uamuzi wa kuvuliwa ubunge baada ya kukiuka Kanuni za kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutokuhudhuria mfululizo vikao zaidi ya vitatu vya Bunge hilo bila taarifa.

Baada ya kuwasilisha maombi hayo Mawakili wa Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Madai anayeshughulikia Katiba, Uchaguzi na Haki za Binadamu Bi. Alecia Mbuya walipinga vikali ombi hilo kwa kuwasilisha hoja zenye mashiko zilizopelekea Jaji aliyekuwa akisikiliza shauri hilo kukubaliana hoja hizo.

Wakiwasilisha hoja hizo Mawakili wa Serikali waliieleza Mahakama Kuu ya Tanzania kuwa madai ya Mhe. Lissu ni batili na hivyo hayastahili kusikilizwa kwa vile yanakinzana na kifungu 5(2) cha sheria ya Rufani kama ilivyorekebishwa na sheria ya marekebisho ya sheria Na.25 ya mwaka 2002.

Aidha Mawakili wa Serikali waliieleza Mahakama kuwa upande wa mlalamikaji haukuwa na haki kisheria kupinga uamzi uliotolewa na Mhe. Jaji Matupa wa kumnyima ridhaa ya kufungua shauri la mapitio ya kiutawala uamuzi halali ambao uliishia kwa Mhe. Lissu kupoteza ubunge wake.

Mawakili wa Serikali waliendelea kuieleza Mahakama hiyo kuwa haikuwa sahihi kupinga maamuzi ya Jaji Matupa kwa njia ya Rufaa kwa kuwa maamuzi hayo hayakumaliza shauri hilo kama ilivyopaswa kuwa kisheria kwa kuwa shauri hilo liliishia katika mapingamizi ya awali.

Mawakili wa Serikali waliendelea kuieleza Mahakama kuwa katika kesi mbalimbali Mahakama ilishaamua kuwa haiwezi kutoa ridhaa ya kukata Rufaa katika shauri ambalo limeishia njiani kama hili hivyo iliamua kulitupilia mbali kwa kuwa maombi haya hayakukidhi vigezo vya kisheria.

Baada ya kusikiliza kwa makini maelezo kutoka pande zote mbili, Jaji aliyekuwa akisikiliza shauri hilo Mhe. Yose Mlyambina alikubaliana na hoja zilizotolewa na mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia ukweli kuwa maombi hayo hayakukidhi vigezo vya kisheria.

Katika shauri hilo upande wa Serikali uliongozwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Madai anayeshughulikia Katiba, Uchaguzi na Haki za Binadamu, Wakili wa Serikali Mkuu Bi. Alecia Mbuya na Wakili wa Serikali Bw. Erigh Rumisha wakati upande wa mlalamikaji uliongonzwa na Wakili wa kujitegemea Bw. Peter Kibatala.

“ ACACIA WAIONA BARRICK NI MKOMBOZI KWA KUINUNUA

10 PAGE

# MAWAKILI WA SERIKALI WATAKIWA KUSIMAMIA MASHAURI KWA KUFUATA SHERIA, KANUNI NA MIONGOZO

Na Dennis J. Buyekwa



Picha ya pamoja katika ufunguzi wa mafunzo kwa mawakili wa serikali.

Mawakili wa Serikali wametakiwa kufuata sheria, kanuni na miongozo wakati wa kusimamia na kuratibu mashauri yote ya Madai, Usuluhishi, Katiba pamoja na Haki za Binadamu yatakayofunguliwa dhidi ya Serikali katika Mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Wito huo umetolewa mapema leo na Bw. Amon Mpanju ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa mawakili wa serikali kwa ajili ya kusimamia Mashauri yote ya Madai, Usuluhisi na Haki za Binadamu yanayofunguliwa dhidi ya serikali.

“Niwasihi mhakikishe kuwa mnatumia mafunzo haya kujiandaa ipasavyo kushiriki kwenye mashauri yatakayojitokeza ili kuhakikisha tunayamaliza kwa muda na kwa ufanisi wa hali ya juu,” alisema Bw. Mpanju.

Bw. Mpanju amewasihi mawakili hao kutumia nafasi hii muhimu waliyoipata kujifunza kwa bidii na kuwa tayari kuiwakilisha vyema Serikali katika mashauri ya Madai, Usuluhishi na Haki za Binadamu wakati wowote mtakapohitajika kufanya hivyo.

“ni matarajio yangu mtafuatilia kwa makini mafunzo haya na kuwa na weledi mzuri wa kusimamia mashauri yatakayojitokeza kwa ufanisi mkubwa,” alisema Bw. Mpanju.




Akizungumza kuhusu wakufunzi watakaotoa mafunzo hayo Bw. Mpanju alisema kuwa Wakufunzi hawa watakaotoa mafunzo haya ni wabobezi wa masuala ya Madai na Usuluhishi hivyo mkiwafuatilia kwa makini, mtapata stadi nzuri za kukabiliana na mashauri yote yanayoyatarajia kufunguliwa katika mahakama mbalimbali.

Naibu Katibu Mkuu aliendelea kuwasisitiza mawakili hao kufuata maelekezo ya wakufunzi hao ili kuhakikisha wanamaliza mafunzo

hayo wakiwa na weledi wa kutosha kufanya kazi zao kwa umakini hatua itakayosaidia kuleta mafanikio makubwa wakati wa uendeshaji wa mashauri hayo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mashauri hayo yanamalizika kwa wakati.

Akizitaja baadhi ya sheria na kanuni mbalimbali zinazosimamia mashauri hayo Bw. Mpanju alizitaja sheria hizo kuwa ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania,1977; pamoja na Sheria ya mwenendo wa madai sura ya ya 33 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Kiongozi huyo pia amewashuru watoa maada katika mafunzo hayo ambao ni Majaji wastaafu wa Mahakama ya Tanzania ambao Mhe. Jaji Mstaafu Dkt. Fauz Twaib pamoja na Mhe. Jaji Makaramba kwa uwezo wao mkubwa wa kisheria pamoja na kuwapa mafunzo Mawakili wa Serikali watakaoshughulikia mashauri yote yanayotarajiwa kufunguliwa dhidi ya Serikali.

Akiwashukuru watoa maada hao Bw. Mpanju emesema nawashukuru sana wote kwa kupanga na kupata nafasi ya kutoa mafunzo haya muhimu kwa Mawakili wetu, hatua hii itatusaidia kurahisisha shughuli zetu za kuendesha mashauri wawapo Mahakamani.

Aidha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha mafunzo haya yenye lengo la kuwajengea uwezo mawakili wa serikali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali Ndg. Gabriel Malata akizungumza wakati wa kumkaribisha mgeni rasmi amesema ili kuhakikisha majukumu hayo yanatekelezwa kwa weledi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inalo jukumu la kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali kwenye maeneo ya mashauri ya Madai na usuluhishi ili waweze kuiwakilisha vyema Serikali ndani na nje ya nchi.

Wakili Mkuu wa Serikali ameongeza kuwa ni matarajio yake kuona kuwa Mawakili wa Serikali waliohudhuria mafunzo hayo watakua wamepata mafunzo yatakayowawezesha kuwa na uelewa wa kesi zote za Madai, Usuluhishi, Katiba na Haki za Binadamu kwa ujumla.

Ameongeza kuwa mafunzo hayo yatasaidia kuwajengea uwezo mawakili hao hatua itakayosaidia kuwaongezea uelewa kuhusu namna bora ya kuandaa nyaraka za Mahakamani, kuelewa wa taratibu zote zinazotumika Mahakamani katika uendeshaji wa kesi mbalimbali, kuelewa ushahidi wa kielektroniki na taratibu zake katika kesi mbalimbali na majukumu ya Mawakili wa Serikali katika kusimamia mashauri hayo.

Ndg. Malata ameishukuru Serikali kwa kufanikisha mafunzo hayo huku akiendelea kuahidi kuwa ofisi yake itaendelea kufanya kazi kwa weledi wa hali ya juu ili iweze kuendelea kuokoa fedha ambazo zinaweza kupotea ikiwa mashauri hayo hayatasimamiwa ipasavyo.

Mafunzo hayo ya siku tatu yanafanyika Jijini Dodoma katika ukumbi wa mikutano wa Kambarage – Hazina, unahusisha Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tamisemi pamoja na Mawakili kutoka katika Wizara mbalimbali za Serikali.









# PROF. MCHOME AHIMIZA UWAZI NA USHIRIKISHWAJI KATIKA UTENDAJI OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Na Dennis J. Buyekwa

Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na sheria Prof. Sifuni Mchome amewataka watumishi wa ofisi ya wakili Mkuu wa Serikali kuzingatia ushirikishwaji katika ngazi zote sambamba na kufanya kazi kwa uwazi, huku wakifuata *"mfuate maadili ya kazi yenu maadili yanakusaidia katika kutekeleza majukumu yako kikamilifu, sekta yenu ni muhimu sheria ikisimama na hata nchi itatulia" amesema Prof. Mchome.*

Amesema mabaraza ya



Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Prof. Sifuni Mchome akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali lililofanyika jijini Dodoma.

miiko ya kazi yao.

Prof. mchome ameyasema hayo leo April 9,2021 jijini Dodoma wakati akifungua Kikao cha pili cha Baraza la wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika Leo April 9,2021 jijini Dodoma amesema kuwa kutokana na unyeti wa ofisi hiyo inahitajika kila mtumishi kufanya kazi wa weredi huku wakilenga kutafuta matokeo.

wafanyakazi ni muhimu sana katika maeneo ya kazi kwa sababu huko ndiko ushirikishwaji utafanyika ni muhimu kila taasisi iwe na mabaraza hayo ambayo yapo kwa mujibu wa sheria.

*"Serikali itahakikisha taasisi zake zote zinatekeleza takwa hili la sheria la kuwa na mabaraza ya wafanyakazi huku ndiko kutafanyika ushirikishwaji katika mambo mbalimbali kwa watumishi katika ngazi zote"* amesema.

Amesema katika majukumu yao wafanye kazi wakilenga kupata matokeo chanya katika kutafuta ushindi katika kesi mbalimbali ambazo wanazisimamia katika ofisi zao zilizopo katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Amewataka kujenga utaratibu wa kufanya tathmini za mara kwa mara katika kazi wanazozifanya ili kuona namna ya kuboresha kazi zao kwani bila tathmini hawawezi kupata kile walichokusudia katika sekta ya sheria hapa nchini.

Ameongeza kuwa "mkasikilize kero za wananchi tunakofanya ziara huko mikoani malalamiko ni mengi, naamini huko mnaofisi zenu mkashughulikie hayo malalamiko ni mengi sana" amesema.

Aidha amewataka wataalamu hao kwendana na kasi ya sasa na sio kufanyakazi kwa mazoea kwani kwa sasa nchi imeingia katika uchumi wa kati hivyo nao wabadilishe namna ya ufanyaji kazi ili kuendana na kasi ya uchumi wa kati ili kama nchi kupata mafanikio zaidi.

Awali Wakili Mkuu wa Serikali ambaye pia ni mwenyekiti wa baraza hilo bw. Gabriel Malata amesema kikao hicho ni cha pili kwa mwaka wa fedha 2020 -2021, ambao wanakutana kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali yanayohusu ofisi hiyo.

Pia amebainisha kuwa ofisi ya wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa Feb, 12, 2018 na aliyekuwa Rais wa awamu ya tano hayati Dkt John Magufuli na kupewa jukumu la kuendesha, kuratibu, na kusimamia mashauri mbalimbali yanayohusu Serikali na taasisi zake.

Amesema katika kipindi cha mwezi julai 2020, hadi Feb, 2021 ofisi hiyo imeshughulikia jumla ya mashauri 3715, kati ya hayo mashauri ya madai ni 3625 na 90 ni ya usuluhishi, jumla ya mashauri 451 kati ya 3715 yaliendeshwa na kumalizika.

Kati ya mashauri hayo 422 ni ya madai ambayo yanajumuisha mashauri 418 ya madai ya ndani ya nchi yakiwamo 13 ya uchaguzi na mashauri manne (4) ya madai ya nje ya nchi, na kukamilika kwa mashauri hayo kumepelekea kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 643.7, ambazo zingelipwa na serikali kama ingeshindwa.

Aidha amesema ofisi hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya kukosa muundo wa uendeshaji wa ofisi hiyo ambapo kwa sasa wanatumia muundo wa ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali.



Baadhi ya Wajumbe wa Baraza waliohudhuria kikao cha Baraza la Wafanyakazi wakifuatilia mijadala mbalimbali iliyojadiliwa katika kikao hicho kama wanavyoonekana kwenye picha




Wakili Mkuu wa Serikali Ndg. Gabriel Malata akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika jijini Dodoma hivi karibuni. Waliokaa kushoto kwake ni Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Prof. Sifuni Mchome pamoja na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace N. Luhende .

# Mama Samia: Nitaboresha Maslahi ya Watumishi

Na Dennis J. Buyekwa

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS), leo tarehe 1/5/2021 imeungana na wananchi duniani kote. katika kusherehekea Sikukuu ya wafanyakazi duniani ambayo imefanyika kitaifa Jijini Mwanza yakiwa na kauli mbiu inayosema, "Maslahi Bora, Mishahara Juu Kazi iendelee!!

Akizungumza wakati wa sherehe hizo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan, ambaye ndiye alikuwa mgeni rasimi amewashukuru wafanyakazi nchini kwa kazi kubwa wanayoifanya huku akiwasihi kuendelea na moyo huo wa kufanya kazi kwa lengo la kuhakikisha wanailetea nchi maendeleo.

Akizungumza kuhusu kuboresha maslahi ya watumishi Mhe.Mama Samia Suluhu Hassani amesema, anatambua mchango na changamoto wanazopitia watumishi huku akiahidi kutatua changamoto hizo ikiwa ni Pamoja na kuboresha maslahi kwa watumishi wa kada zote kwa lengo la kuwaongezea motisha watumishi.

Wakizungumza mara baada ya sherehe hizo watumishi walioshiriki sherehe hizo, waliishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwaruhusu kushiriki maadhimisho hayo kwani inawasaidia kutengeneza mahusiano mazuri na watumishi wenzao kutoka taasisi nyingine ikiwa ni Pamoja na kubadilishana ujuzi wa namna wanavyotekelza majukumu yao ya kila siku.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imefanikiwa kushirirki sherehe hizo kikamilifu kupitia Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE), ambapo watumishi waliohudhuria sherehe hizo walifanikiwa kupita kwa maandamano mbele ya Mhe. Rais huku wakiwa na mabango yenye kauli mbiu ya sherehe hizo ikiwa ni ishara ya kuonyesha kuwa wako Pamoja naye katika jukumu zima la kuletea nchi maendeleo.

Siku ya Mei Mosi Duniani ilianzishwa Karne ya 19 nchini Marekani, kutokana na mgomo mkubwa wa wafanya kazi uliotokea nchini Marekani mwaka 1827 wakidai mabadiliko ya muda wa kufanya kazi, na baada ya hapo imekuwa ikiadhimishwa kila mwaka duniani kote.




MEI MOSI
Mwanza 2021
SEKTA YA UCHUKUZI
UCHUKUZI SPORTS CLUB
MICHEZO HULETA AFYA, MSHIKAMANO
NA UFANISI MAHALA PA KAZI
MEIMOSI - 2021, MWANZA
Mei Mosi
Mwanza 2021





# PROF. KILANGI ATAKA MAWAKILI NCHINI KUJINOA KILA UCHAO

Na Dennis J. Buyekwa

Mawakili wa Serikali nchini wametakiwa kuendelea kujielimisha kila siku kutokana na kukua kwa taaluma ya Sheria ili kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yao, hatua itakayo wasaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi Zaidi.

Wito huo ameutoa leo Juni 14,2021 jijini Dodoma na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati akifungua mafunzo ya siku nne yenye lengo la kuwajengea uwezo Mawakili wa serikali kwenye uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi yaliyoandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Profesa.Kilangi amesema kuwa mafunzo hayo ni muhimu na yatasaidia kuwanoa Mawakili hao ili kuendana na mabadiliko ya taaluma ya Sheria ambayo yamekuwa yanatokea kila siku ulimwenguni kote.

"Mafunzo haya ni kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi na weledi katika utekelezaji wa majukumu yenu na kuboresha mahusiano jambo ambalo ni muhimu katika utendaji kazi, mada muhimu zitagusiwa ni Pamoja na weledi katika uendeshaji wa mashauri ya madai," amesema Profesa.Kilangi.

Profesa.Kilangi amesisitiza kuwa mada hizo ni muhimu kwao katika uendeshaji wa mashauri ya serikali kwani kupitia maada hizo mawakili watakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuweza kukabiliana na shauri lolote litakalofunguliwa dhidi ya serikali ndani na nje ya nchi.

"Lazima muwe na ujuzi wa kusimamia na kuendesha mashauri haya kwa weledi ndani na nje ya nchi inaweza kuwa kwenye Mahakama za Kimataifa au Mabaraza ya kimataifa," amesema Prof.Kilangi

Pia ameitaka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kushirikiana na Taasisi mbalimbali katika kutatua Changa moto mbalimbali zinazoikabili ofisi hiyo ikiwemo uhaba wa mawakili wa Serikali hatua itakayoiongezea ufanisi ofisi hiyo muhimu.

Kwa upande wake Wakili Mkuu wa Serikali, Ndg. Gabriel Malata ,amesema ofisi hiyo ilipewa jukumu la kuendesha madai ya kesi ndani na nje ya nchi na kupitia mafunzo hayo yanaenda kuwaweka katika mtazamo mmoja wa uendeshaji wa mashauri kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake huku akibainisha mafanikio na changamoto mbalimbali.

Ndg. Malata amesema kuwa ndani ya miaka mitatu Ofisi yake imeokoa zaidi ya Sh.Trilioni 12 katika mashauri ya madai yaliyokuwa yamefunguliwa dhidi ya serikali.

Amesema kuwa ofisi hiyo ilianza kutekeleza majukumu yake mwaka 2018 na kwa kipindi hicho mafanikio mbalimbali yamepatikana ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/20 ofisi hiyo ilifanikiwa kuokoa fedha ambazo zinatokana na mashauri yaliyofunguliwa dhidi ya serikali na taasisi zake kiasi cha Shilingi takribani Trilioni 11.4.

Ofisi ya Wakili Mkuu pia ilifanikiwa kuendesha

mashauri mbalimbali ambayo hayahusishi fedha na kufanikiwa kurejesha mali mbalimbali za serikali ikiwamo mashamba 106 pamoja na Hoteli iliyokuwa imetwaliwa kinyemela na watu wenye nia mbaya dhidi ya serikali.

Akielezea changamoto zinazoikabili Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Ndg. Malata amezitaja changamoto hizo kuwa ni uhaba wa mawakili ambapo mpaka sasa ofisi hiyo inao mawakili 88 tu huku mahitaji halisi ya Mawakili ikiwa ni Mawakili 308, uhaba wa watumishi kutoka kada nyingine pamoja na vitendea kazi mbalimbali ikiwemo magari kwa ajili ya kupeka Mawakili Mahakamani














# WAZIRI KABUDI: TOENI TAARIFA KWA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Na Dennis J. Buyekwa

Waziri wa Katiba na Sheria,Profesa Paramagamba Kabudi ametoa wito kwa mawakili wa serikali ambao wamekuwa wakisimamia mashauri mbalimbali ya serikali kutoa taarifa kwa Ofisi ya wakili mkuu wa serikali na siyo kusubiri hadi mambo yawe magumu.

Prof. Kabudi ametoa wito huo leo June 18,2021 jijini Dodoma wakati akifungua mkutano mkuu wa watumishi wa Ofisi ya Wakali mkuu wa serikali ambapo amesema Mawakili wote wa Mashirika ya umma lazima wawajibike kwa Wakili Mkuu wa Serikali.

*"Mawakili wote wa mashirika ya umma lazima wawajibike kwa Wakili mkuu wa serikali na kesi zote lazima waripoti kwa Wakili mkuu siyo kusubiri hadi mambo yanapokuwa magumu ndiyo wanaripoti"* amesema Prof. Kabudi.

Aidha,Waziri Kabudi amesema kuwa ipo haja ya kuimarishwa kwa Ofisi ya Wakili mkuu wa serikali ili kusaidia kusimamia mashauri yote yanayoikabili serikali ndani na nje ya nchi hatua itakayosaidia serikali kupata haki zake kwa wakati.

Prof. Kabundi amesema kuwa kwa kufanya hivyo itasaidia kuiondolea mzigo Serikali wa gharama kubwa ya fedha ambayo imekuwa ikitumia kwa ajili ya kulipa mawakili hasa wale wa nje ya nchi na badala yake fedha hiyo ielekezwe kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kiongozi huyo ameongeza kuwa ipo haja ya serikali kuwa na taasisi ya mafunzo ya mawakili wa Ofisi ya serikali ambayo itatumika kutoa mafunzo ya mara kwa mara ili kuimarisha utendaji kazi wao kwa kuwa mawakili wanapaswa kujielimisha muda wote ili waweze kuwa tayari kukabiriana na shauri lolote litakalojitokeza wakati wote.

Amesema hali hiyo italisaidia taifa kuondokana na matumizi makubwa ya fedha kwa ajili ya kulipa mawakaili wa nje pale taifa linapofunguliwa mashauri mbalimbali nje ya nchi, alieleza kuwa badala ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo baadala yake fedha hizo zimekuwa zikitumika kwa ajili ya kuendeshea mashauri mbalimbali ambayo yamekuwa yakifunguliwa dhidi ya serikali.

*"Hawa viongozi wetu Mama Samia hata wakati ule wa Hayati Dkt. Magufuli wanapata shida sana unakuta wametenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye miundombinu au miradi ya maendele lakini unakuta nchi inashitakiwa na kwenda mahakamani hivyo serikali imejikuta ikitakiwa kutumia fedha nyingi sana kulipa mawakili wanaoendesha mashauri hayo,"* amesema Prof. Kabudi.

Aidha Waziri Kabudi amesema kuwa, mashauri ambayo yamekuwa zikifunguliwa yanailazimu nchi kulipa mamilioni ya fedha ambayo yangetumika katika miradi mingine ya maendeleo kama ujenzi wa reli ya

kisasa ya umeme (SGR), vituo vya afya nchi nzima, bwawa la umeme la Nyerere Pamoja na Pamoja na miradi mingine ya maendeleo.

“Hivi sasa tunapitia kipindi cha mpito lakini baadaye nataka ofisi hii ndiyo iwe inasimamia mashauri yote ya ndani na nje yanayofung7uliwa eitha na Serikali au dhidi ya serikali naamini kwa kufanya hivi tutafanikiwa tuu kama tutaendelea kuimarisha Ofisi ya Wakali mkuu wa serikali,” amesema Prof. Kabudi.

Kwa upande wake, Wakili Mkuu wa serikali, Ndg. Gabriel Malata,ameiomba Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kuendelea kuwapatia mafunzo mawakili hao ili kuendelea kuwajengea uwezo katika uendeshaji wa mashauri madai na usuluhishi katika sekta ya Gesi na Madini ili mawakili hawa waweze kuiwakilisha serikali ipasavyo hasa ukizingatia ukweli kuwa sasa nchi inaelekeza katika uchumi wa kati wa juu na wanasheria wengi hawana uelewa wa kutosha katika sekta hiyo.

Ndg. Malata ameongeza kuwa wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa watumishi 312 ambapo amedai waliopo ni 143 hivyo ameiomba Serikali kuwasaidia watumishi Zaidi ili OWMS iendee kutekeleza majukumua yake kwa weledi zaidi.

Mkutano hucho ulioandaliwa na OWMS umewahusisha watumishi wote wa ofisi hiyo kutoka mikoa kumi na sita 16 nzima na hapo kabla ulitanguliwa na mafunzo ya siku nne yaliyokuwa na lengo la kuwajengea uwezo Mawakili wa serikali kutoka OWMS, TAMISEMI na Mashirika ya Umma katika uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi.













## SERIKALI YADHAMIRIA KUPATA UFUMBUZI WA KUDUMU UHABA WA WATUMISHI KATIKA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Serikali kupitia Waziri wa Katiba na Sheria imesema, imeazimia kuendelea kuimarisha taasisi zote za utoaji haki hasa Mahakama pamoja na kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo, hususani uhaba wa watumishi huku ikiwataka Wanasheria wote wa umma nchini kuhakikisha wanafanya mashauriano na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kabla ya kuanza kuendesha na kusimamia mashauri ya serikali.

kauli hiyo Imetolewa jijini Dodoma mapema leo na Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Paramagamba Kabudi wakati akifungua mkutano wa kwanza wa Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kusema Serikali itahakikisha inazifanyia kazi changamoto zote zinazoikabili ofisi hiyo ili kuhakikisha inajenga mazingira Rafiki kwa watumishi wake.

Aidha, amesema katika kufanya mashauri yote kupitia ofisi ya wakili wa Serikali itasaidia wao kujipanga kisheria katika mashauri yao.Waziri Kabudi ameeleza hali hiyo itasaidia Taifa kuondokana na matumizi makubwa ya fedha kwa ajili ya kulipa mawakili wa nje pale Taifa linapofunguliwa mashauri nje ya nchi kwa kuwa nchi imekuwa ikitumia fedha nyingi kuendesha mashauri hayo.

"Nipende kuwaeleza hivi sasa tuendelea tu na hiki kipindi cha mpito, lakini baadaye nataka ofisi hii ndiyo iwe inasimamia Mashauri yote za serikali yale ya ndani na nje tutafanikiwa kama tutaendelea kuimarisha Ofisi hii ya Wakali Mkuu wa Serikali," amesema Profesa Kabudi.

Hata hivyo amewataka mawakili wa mashirika ya umma ambao wamekuwa wakisimamia kesi mbalimbali kutoa taarifa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na siyo kusubiri hadi hali inapokuwa mbaya. amesema, ipo haja ya kuwa na taasisi ya mafunzo kwa Mawakili wa Serikali ambayo itatumika kutoa mafunzo ya mara kwa mara ili kuimarisha utendaji kazi wao.

Katika hatua nyingine Waziri Kabudi, ametaka kuona umuhimu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mahakama hapa nchini kwa kuweka istilahi na misamiati ya kisheria katika suala zima la uendeshaji mashauri mbalimbali nchini.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali,Bwa. Gabriel Malata ameiomba Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kuandaa programu za mafunzo ili kuwajengea uwezo Mawakili wa serikali katika uendeshaji wa madai ya Gesi na Madini katika kuelekea uchumi wa Viwanda kutokana na wanasheria wengi hasa wa serikali kutokuwa na uelewa wa kutosha katika sekta hiyo.

Akielezea kuhusu changamoto nyingine zinazoikabili Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Ndg. Malata alizitaja changamoto hizo kuwa ni Pamoja na uhaba wa vitebdea kazi ikwemo suala la upungufu wa Watumishi, Magari machache Pamoja na upungufu wa ofisi za mikoani.

"Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa sasa inakabiliwa na upungufu wa watumishi ambapo kwa sasa ofisi inaowatumishi 143 wakati mahitaji halisi ni watumishi 312 wakati kuhusu magari ofisi inayo magari 15 ambayo hayakidhi mahitaji ya ofisi kwa sasa". Alisema Ndg. Malata.





# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YAKUMBUSHWA KUZINGATIA KANUNI, TARATIBU, MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Na Dennis J. Buyekwa

Viongozi wa ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wamekumbushwa umuhimu wa kufanya kazi kwa kufuata na kuzingatia Kanuni, Taratibu, Maadili ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora protokali na Mawasiliano ikiwa ni hatua itakayosaidia kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.
Wito huo umetolewa na Wakili Mkuu wa Serikali Ndg. Gabriel Malata wakati akifungua mafunzo ya siku nne (4) yenye lengo la kuwajengea uwezo Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na kuwakumbusha umuhimu wa kufanya kazi kwa kufuata Kanuni, Taratibu, Maadili ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Protokali na Mawasiliano.
Wakili Mkuu wa Serikali aliendelea kuwakumbusha wajumbe hao kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa upendo na amani miongoni mwa watumishi kwa kuwa itasaidia kujenga mshikamano na ushirikiano uliopo miongoni mwa watumishi ofisi hapo hatua itakayosaidia kuongeza fanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.
Aliwaagiza wajumbe hao pia kuhakikisha wanawasimamia vyema watumishi walioko chini yao huku wakiwapa ushirikiano pale wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku kwani kwa kufanya hivyo itasaidia kuweza kuwajengea uwezo hatua itakayosaidia watumishi hao kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Akizunguza mtoa maada wa kikao hicho Ndg. Bw. Mluli Mahendeka watumishi wanalo jukumu kubwa la kutunza siri za serikali hasa kwa yale masuala muhimu yenye maslahi mapana ya taifa, sambamba na hilo wajumbe hao pia walikumbushwa umuhimu wa kulinda mali za serikali kwa kuelezwa kuwa jukumu la kulinda mali za serikali linaanza na mtumishi mwenyewe kwa kuwa taarifa nyingi za ofisi anazo kichwani mwake.
Wakati wa kikao hicho aliwakumbusha wajumbe kuwa usalama na uendeshaji wa shughuli za serikali kwa kiasi kikubwa unamtegemea mtumishi wa umma bila kujali nafasi yake, kwa kuwa vifaa na nyenzo za uendeshaji wa shughuli zake za kila siku vinasimamiwa na mtumishi mwenyewe. Hivyo, watumishi walikumbushwa umuhimu wa kuwa makini na vitendea kazi vyao ikiwa ni pamoja na kutunza siri za serikali ili serikali na mali zake ziendelee kuwa salama wakati wote.
aliwakumbusha wajumbe wote juu ya umhimu wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria za nchi ili kuhakikisha maslahi ya nchi yanalindwa kwa nguvu muda wote na kutekeleza majukumu yao kwa weledi usiotiliwa shaka kwa namna yoyote ile.
Akizungumza katika kikao hicho Mkuu wa Takukuru mkoa wa Temeke Bw. Donasian Kessy alisema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wanaowajibu

wa kuhakikisha wanapambana na vitendo vyote vinavyosababisha rushwa kwa kuzingatia kuwa rushwa ni adui wa haki.

"wajibu wa kupambana na rushwa ni jukumu la kila mmoja, kwa kuwa kila mwananchi anaowajibu wa kutoa taarifa juu ya vitendo vya rushwa." alisema Bw. Kessy.

Aliongeza kuwa, sambasamba na kutekeleza majukuu yao bila upendeleo, woga, ubaguzi wala huba ya aina yoyote. Vilevile watumishi wanawajibika kutojihusisha na vitendo vya rushwa Pamoja na kulinda Tunu za zaifa ambazo ni uhuru, amani na umoja.

Wajumbe wa Menejimenti ya OWMS walikumbushwa kuwa ili kuhakikisha wanapambana na vitendo vya rushwa ni wajibu wao kama viongozi wa ofisi kuhakikisha wanakuza uzalendo miongoni mwa watumishi wanaowasimamia, ikiwa ni Pamoja na kubadilisha fikra za watumishi wa OWMS sambamba na kuwahamasisha watumishi hao kutekeleza majukumu yao kwa upendo, amani, uadilifu na kufuata maadili ya utumishi wa Umma, utawala bora Pamoja na Haki za binadamu.

Nao wajumbe waliohudhuria mafunzo hayo wameishukru ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwaandilia mafunzo hayo kwa kusema kuwa mafunzo hayo ni muhimu na yamekuja muda mwafaka kwani yatasaidia kuwarahisisishia utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku, huku wakiiomba ofisi hiyo kuandaa mafunzo mengine kama hayo kwa lengo la kuwaongezea uelewa wa masuala mbalimbali.

Maada nyingine zilizotolewa katika wakati wa kikao kazi hicho ni Pamoja na umuhimu wa Mawasiliano mahala pa kazi, Majukumu ya Viongozi wa Umma katika Usimamizi wa Utumishi wa Umma, Itifaki na Etiquette Pamoja na elimu kuhusu Masjala Mtandao.





# TANZIA



Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inasikitika kutangaza kifo cha Mtumishi wake Bi. Judith Mawi (Mwandishi Mwendesha Ofisi) kilichotokea tarehe 25/02/2021 nyumbani kwake Boko Basihaya - Dar es Salaam.






# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 1902
41218 DODOMA
Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)
Barua pepe: dodoma@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 130
31101 MUSOMA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: mara@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 1280
63114 MTWARA
Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara
Barua pepe: mtwara@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 394
33101 MWANZA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: mwanza@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 595
51108 IRINGA
Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa
Barua pepe: iringa@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 106
35102 BUKOBA
Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Muhakiki Mali
Barua pepe: kagera@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 564
57101 SONGEA
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 43
37101 SHINYANGA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 60
21101 TANGA
Jengo la Bandari
Barua pepe: tanga@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 119
45112 TABORA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: tabora@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 202
25101 MOSHI
Jengo la TRA Moshi
Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 321
55103 SUMBAWANGA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: rukwa@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 66
23101 ARUSHA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barau pepe: arusha@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 710
53107 MBEYA
Jengo la Madini
Barua pepe: mbeya@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 172
47101 KIGOMA
Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma
Barua pepe: kigoma@osg.go.tz

osgtanzania

osg_tanzania